# WAJIBU WA KANISA KWA MTOTO

IDARA YA ELIMU SOUTH NYANZA CONFERENCE



*“Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo, si kwa kutaka fedha ya aibu bali kwa moyo. Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee, Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.”*

**— 1 PETRO 5:2,5.**

# UTANGULIZI

Kanisa la Waadventista wasabato linamtambua Mungu kama mwasisi wa uhai, ukweli na uwezo. Kabla ya dhambi kuingia Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake akiwa mkamilifu, ila dhambi ikaharibu mpango mzima na mahusiano mema yaliyokuwepo kati ya Muumbaji na kiumbe chake (mwanadamu). Hivyo shule za kanisa tangu agano la lake na agano jipya, Mungu amezipatia jukumu la kurudisha yale mahusiano halisi yalikokuwepo tangu mwanzo kabla ya dhambi kuingia duniani. Ndio maana kusudi kubwa la kuwa na shule za kanisa ni kumrejesha mwanadamu katika sura ya Mungu aliyoipoteza.



# UTANGULIZI

Hili linawezekana kwa kukubali uongozi wa roho mtakatifu kutawala shule zetu. Hata hivyo utafiti umeonyesha kuwa washiriki waliopata elimu katika shule za kanisa wamekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza utume wa kanisa kwa vipaji na ujuzi Mungu alivyowapatia. Zaidi ya yote, watoto waliotumia muda mwingi kupata Elimu katika shule za kanisa ndivyo walivyoendelea kulipenda kanisa Zaidi na kutumia karama zao kwa kazi ya Bwana. Amaa kweli, "Mlee mtoto katika njia impasayo naye hata iacha hata atakapokuwa mzee (Mithali 22:6).



# **WAJIBU WA KANISA** KWA MTOTO

- Wajibu wa kwanza wa kanisa kwa mtoto ni kumuonyesha mtoto upendo wa Mungu na kuukubali ( Yoh 3:16) “ kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanae wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”.

- Wajibu wa pili wa kanisa ni kuwapatia watoto wa kiadventista malezi endelevu ya kiroho. Jukumu hili ndilo linalolisukuma kanisa kuanzisha shule zake na kuimarisha watoto na vijana wetu kiroho na kuwaandaa kwa ajili ya kuja kwa Kristo mara ya pili. Jambo ambalo linawawezesha watoto wetu kuwa na mwendelezo wa kumjua Mungu, kumwamini na kumwabudu.

# **WAJIBU WA KANISA** KWA MTOTO

- Wajibu wa tatu wa kanisa ni kuwapatia watoto wetu kanuni za maisha, imani, mitazamo, maadili, tabia na desturi za kanisa lao ili walielewe kanisa na kudumu humo, kanisa likiwasaidia watoto wetu kuakisi makuzi ya Yesu ambayo yanapatikana katika kitabu cha Luka 2:52 " Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo , akimpendeza Mungu pamoja na wanaadamu". Ndio maana kanisa la waadventista wasabato lina idara mbalimbali ndani ya kanisa ikiwe idara ya vijana na idara ya watoto kwa ajili ya malezi ya vijana wetu na watoto wetu.

- Wajibu wa nne wa kanisa ni uinjilisti. Kanisa lina wajibu wa kuwaandaa watoto wetu na vijana wetu kuitikia wito wetu mkuu wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa yesu, na kuwabatiza kwa jina la Baba , na Mwana , na Roho mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote Yesu aliyotuamuru, na tazama mimi niko pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.

# BARIKIWA!

Kwa Maoni, Maswali na Ushauri;
Wasiliana nami kwa email;
mlingwamarco@gmail.com




PR. MARCO F. MLINGWA